

## **WARSHA YA KWANZA YA ATHARI ZA MABADILIKO YA TABIANCHI**

### **SAFARI YA MKOA WA KAGERA KUELEKEA KUJIPANGA UPYA KUKABILI NA KUZUIA ATHARI ZA MABADILIKO YA TABIA NCHI.**

#### **ITAFANYIKA WILAYANI BUKOBA MARUKU PARADISE BEACH**

**TAREHE 20 NOVEMBER 2021**

**Muda huu mkutano mkubwa wa umoja wa mataifa utakaokuwa umehudhuriwa na viongozi 190 wa achi za dunia ambapo Tanzania ni mjumbe COP26 huko Uingereza kati ya tarehe 1 -12 November 2021 ndio utakuwa umekamilika. Hivyo tutaangalia pia maazimio ya mkutano huu kuhusu jinsi ya kuyakabili majanga ya mabadiliko ya tabianchi.**

**MWANDAAJI NA MWENDESHAJI WA WARSHA :** Mama Mary Kalikawe, ambaye ni mwanamazingira mwandamizi na mshahuri mzoefu wa Sekta ya utalii.

**MGENI RASMI:** Mkuu wa Mkoa Kagera

**MADA KUU YA WARSHA:** Kuanzisha mazungumzo na mikakati ya kuzikabili athari na maswala ya mabadiliko ya Tabianchi katika mrengo wa mazingira ya mkoa wa kagera na nchi yetu Tanzania.

**DIRA:** Kagera kwa kupitia wadau itajipambanua kama mkoa ambao unatafuta mfumo wa uchumi utakaoyakabili mabadiliko ya Tabianchi na kuzuia ukuaji wa athari hizi wakati maendeleo endelevu yakipatikana kupitia uchumi wa hewa ukaa ya chini yenye ulinganifu.

#### **KWA NINI IWEPO WARSHA HII:**

1. Kuanzisha mazungumzo ya wazi juu ya mabadiliko ya tabianchi katika jamii ya wana Bukoba/Kagera ambayo yatakua na kuongeza msukumo kwenye muda ulio mbele yetu.
2. Kukuza uelewa kuwa mabadiliko ya tabianchi maana yake ni nini kwa washiriki wa warsha na kuwawezesha wajisikie kuwa kwa kufanya kazi pamoja tutaleta mabadiliko tunayoyataka.
3. Kuandaa list ya matendo chanya katika kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi katika mkoa wetu na kujitoa kuanza kuyatimiza ili kuunga mkono majitoleo yatakayofanywa na serikali ya Tanzania katika mkutano wa COP26

#### **WALENGWA/ WASHIRIKI WA WARSHA**

1. Wadau katika sekta za fedha, mabenki, hali ya hewa na wanasayansi
2. Wanamipango/ watoaji wa maamuzi katika maswala ya mazingira, Utalii, Kilimo, Uvuvi, Miundombinu na afya
3. Biashara ambazo masoko yao ya wateja yataathiriwa kwa mfano nishati, usafirishaji, mnyororo wa ugavi wa utalii kama mahoteli, nk.

4. Vyuo na elimu ( kwa wanafunzi kuelewa maswala ya ongezeko la joto duniani na hatari zake na wakati huo huo kujisikia wana uwezo wa kushiriki kwenye kubadilisha mambo ili kesho yao iwe salama.)
5. Wabunifu na wajasiria mali ambao watajitoa kutafuta njia mbali mbali za ufumbuzi wa janga la mabadiliko ya tabianchi kwa mazingira ya mkoa wetu wa Kagera na Tanzania kwa ujumla.
6. Wawakilishi wa jamii na wadau, wakiwemo wenye ujuzi wa asili wa jinsi ya kukayakabili mazingira kwa njia anuai na endelevu.

#### **RATIIBA YA WARSHA**

MUDA/SAA	MADA	WAHUSIKA
2:00 Asubuhi	Washiriki kuwasili maruku Paradise Beach na kuhakiki usaili wao kwenye warsha	Wote
3:00	Kujitambulisha	Wote
3:10	Mpangilio wa warsha na matokeo yanayotarajiwa	Mary Kalikawe
<b>SEHEMU YA KWANZA</b>	<b>MABADILIKO YA TABIA NCHI NA MAANA YAKE KWA TANZANIA NA MKOA WA KAGERA</b>	
3:20	Mabadiliko ya Tabianchi ni nini? Kuongezeka kwa joto la dunia ni nini? Kwa nini hili ni janga la dunia na wanaadamu? Je viongozi wa dunia wanafanya nini juu ya janga hili?	Mwana Mazingira
3:30	Maswali na majibu	Mwenyekiti wa warsha
4:00	Hotuba ya Mgeni Rasmi: Kwa nini mkoa wa Kagera unahitaji uchunguzi juu ya aina za athari zitakazotokana na mabadiliko ya Tabianchi, mikakati ya kuyakabili yakitilia maanani mazingira mahusisi ya mkoa huu, mali asili zilizopo, hali ya hewa maisha ya jamii husika na mifumo yao ya maisha.	Mgeni Rasmi
4:30	PICHA YA PAMOJA NA CHAI	
<b>SEHEMU YA PILI JE TUNaweza KUFANYA NINI LEO KUYAKABILI MABADILIKO NA KUZUIA YASIEENDELEE?</b>		
5:00	Africa/Tanzania: Mifano ya jinsi watu na mashirika mbali mbali yanavyofanya ikiwemo upandaji wa miti, kurudisha bioanuai, malipo ya mikopo ya carbon na mipango ya utalii. Kuhuisha na matokeo ya COP26	

5:20	Mfano mahususi : Majadiliano kuhusu athari za kujaa kwa ziwa Victoria na uchafuzi wa mazingira kwenye jamii , biashara, samaki wa ziwa na mito, na wanyamapori. Je tunaweza kufanya nini kama mtu mmoja mmoja kuupanga upya mfumo wa uchumi wa mkoa wa Kagera na ustawi wa jamii yake? Kuhuisha na matokeo ya COP26	Mwenyekiti wa Warsha
5:50	Kutengeneza list ya mambo ya kufanya juu ya ziwa Victoria	“
<b>SEHEMU YA TATU FURSA ZILIZOPO NA HATUA ZITAKAZOFUATA IKIHUIHWA NA MATOKEO YA COP26</b>		
6:10	Tanzania kama mwanzilishi wa namna ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi uvumbuzi na ubunifu ikiwemo kutumia ujuzi wa ...	
6:35	Je mabadiliko ya Tabianchi yataleta fursa zipi?	
6:50	Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kukabiliana na kuzuia mabadiliko ya tabianchi	
7:05	Majadiliano katika vikundi na makubaliano juu ya list ya mambo ya kufanya kama mtu mmoja mmoja na kwa pamoja kwa mazingira ya Bukoba na mkoa wa Kagera.	
7:45	Makubaliano na maazimio	
8:00	MWISHO WA WARSHA NA CHAKULA	
	KUENJOY BEACH NA MICHEZO YA BEACH	
11:00 Jioni	Usafiri kuondoka kurudi mjini Bukoba	